Mashahidi Kwa Ajili Ya Bwana

(Witnesses For The Lord)

Na

Ellis P. Forsman

Mashahidi Kwa Ajili Ya Bwana

(Witnesses For The Lord)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 21, 2016

Mashahidi Kwa Ajili Ya Bwana

Luka 12:48

Ni Nani Aliyeshahidi Kwa Ajili Ya Bwana?

Ni nani anayeweza kuwa na sifa kama “shahidi” wa Bwana?

Kulikuwa na watu waliochaguliwa kama mashahidi wa Kristo katika karne ya kwanza. Yesu anaweka wazi katika Luka 24:48 na Matend. 1:8.

- Luka 24:48, “*Ninyi ni mashahidi wa mambo haya.*”
- Matend. 1: 8, “*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu kwanzia Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi.*”

Sasa, swali ni,je haya maandiko yanazungumzia wewe na mimi leo?

Mimi sikuwepo wakati Yesu alipofufuka na kuonekana, ambayo imezungumziwa katika Luka 24: 48, Yesu alipowachagua baadhi ya wanafunzi kama mashahidi wa mambo hayo. Au wewe ulikuwepo?

Sikuwa katika mlima wa mizeituni siku hiyo kuu ya kupaa kwake, alipowaita wanafunzi wake kuwa mashahidi wake. Je ulikuwepo? Hakika haukuwepo!

Vile vile, kuna watu maelfu waaminifu leo ambao wanafikiria wao wenyewe kuwa wa kisasa ambao ni mashahidi wa Mungu na Yesu.

Wengi wanavyo dai kuwa ni mashahidi wa Mungu na Yesu si mashaidi wazuri sana wakati Biblia inatumika kwa ushahidi.

Lakini, kuna ushahidi wa ubora gani ambao unaweza kuwa, tofauti na neno la Mungu lililovuviwa?

Mashahidi wa leo wa Mungu na Yesu Kristo kila mara hawataukubali uvuvio wa neno la Mungu la kipekee, ambayo kila mara inapingana na mambo yao binafsi, ushahidi wao ambao haujavuviwa.

Mara nyingi, mashahidi kama hao kimsingi wanakataa ushahidi wa Mungu kwa sababu ya hatari yao binafsi! Kwa nini mtu apendezewe na ushahidi ambao ni wa uongo kwa Mungu!

Ushahidi Uliokosewa

Leo, watu wengi wazuri wanaweza kujivuna wenyewe kuwa wao ni mashahidi wa Kristo, lakini hawajui chochote kuhusu Biblia; bado wanafikiria kutoa ushahidi kwa watu kuhusu Bwana

Baadhi ya "mashahidi" hawawezi kukaa na kuzungumzia Biblia kiundani, au kutafuta mandiko, hasa kama kifungu cha Biblia haipo katika dondoo zao za vichwa na kuyasema ambayo yanaweza kutumika na kuwa fanya watu waamini kwamba wao ni mashahidi wa Mungu.

Nimewahi kuwa na nafasi ya kuongea na watu wazuri waliofikiria kwamba wao ni mashahidi wa Mungu na Yesu Kristo, lakini tulipoangalia Biblia kwa ajili ya ushahidi uliovuviwa, kutoka katika ushahidi bora walithibitisha kuwa ni ushahidi mbaya, wakijua kidogo kuhusu ushahidi takatifu kutoka katika ushahidi wa kweli uliofunuliwa katika Biblia.

Mashahidi wa kweli wa Bwana walitambulika na Biblia- karibia miaka 2000 iliyopita. Hudhani kuwa ni kitu kigeni kwamba baadhi ya mashahidi waliokosewa waki dhiirisha kile kinachoitwa ujuzi wa kidini ambayo walikuwa nayo **siku chache badaye**? Na ushahidi wao ulikuwa katika mgongano wa moja kwa moja na ushahidi takatifu iliyofunuliwa katika Biblia

Nataka kuleta baadhi ya maswali kwako ili ufikirie!

- Leo hii tunawatu wa kisasa ambao ni mashahidi wa Kristo?
- Kuna mtu yeyote anayeishi leo hii aliyewahi kumuona Yesu, ili kwamba awe shahidi wake wa kweli?
- Je watu leo wako katika nafasi ya kuwa mashahidi wa Kristo, jinsi tunavyoona katika Biblia?
- Wakati ushahidi wa kisasa wa Mungu au wa Yesu wakiwa katika kupingana moja kwa moja na ushahidi ulioko katika Biblia, wewe utachagua upi?

Kuna kitukimoja kukihusu, ushahidi wa Mungu iliyofunuliwa katika Biblia haiwezi kubadilishwa. Mungu hawezi kusema uongo!

Ni vizuri kwa muda huu kuzingatia baadhi ya tafsiri ya somo hili katika uchunguzi.

Ndg. Thayer katika kamusi ya Kiingereza na Kiswahili anatoa tafsiri ya shahidi: "kuwa shahidi, kutoa ushahidi, kushuhudia, kuthibitisha kwamba mtu ame wahi kuona au kusikia au kuwa katika hali ya kitufulani, au kwamba anaijua kwa sababu inafundishwa na ufunuo

uliovuviwa au uvuvio.....kutoa ushahidi....kuthibitisha au kuhakikisha kwa ushahidi."

W. E. Vine katika "kamusi yake ya maneno ya Agano Jipya kiitwacho kiitwacho Expository anatafsiri shahidi wa kweli: "Anayechangia au anasema kile ambacho ameona au kusikia au anajua."

Hakika, tunaweza kufahamu kuwa mitume na mashahidi wa macho wa karne ya kwanza walikuwa ni mashihidi wenye sifa wa Bwana. Lakini, kiukweli, hujui kwamba hakuna mtu katika dunia hii ambaye anasifa ya kuwa mashahidi kama hao wa kwanza walivyo kuwa! Ambaye sasa anaishi aliyemwona Bwana?

Mashahidi Wa Kristo

Sasa hebu na tuangalie jinsi neno "mashahidi wa Kristo" linavyo tumiwa katika Biblia.

Yesu alitumiaje neno hili? Hakika alijuwa neno hili lilimaanisha nini na sifa zake ziliitaji nini.

Kulingana na Yohana 15:27, Yesu alisema, "*Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja name.*"

Sasa mashahidi wa leo wamemuona, kama mitume walivyo mwona miaka 2000 iliyopita? Je mashahidi hawa wa sasa wamewahi kuwa na Yesu toka mwanzo?

Oh, ndiyo, kuna watu leo wanaofikiria kwamba kila kitu katika Yohana, sura ya 14, 15 na 16, inawazungumzia wao, sawa na jinsi ilivyowaongelea mitume katika karne ya kwanza.

Lakini kwa hakika huu ni uongo, kwa sababu hakuna mtu leo hii ambaye amewahi kuwa na Yesu tokea mwanzo wa huduma yake binafsi, kama jinsi walivyokuwa mitume.

Baadhi wame hitimisha kuwa Yohana 5:32 inatoa uthibitisho sahihi wa "mashahidi" leo.

Yohana 5:32, "*Yuko mwingine anayenishuhudia; name najua ya kuwa ushuhuda wake anaonishuhudia ni kweli.*"

Andiko hili halitowi ufafanuzi kwa kile kinachoitwa "kushuhudia" wa leo. Katika misitari inayoendelea Yesu anaonyesha kuwa alikuwa akisoma akili za Mafarisayo kwamba walifikiria kwamba Yesu alikuwa anajizungumzia yeye binafsi kwamba alikuwa mwana wa Mungu, ushahidi wake yawezekana ikawa kweli.

Yohana 5:30-31, "*Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na huku yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka. Mimi nikijishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu si kweli.*"

Yesu alikuwa na mambo mengi kwamba maneno yake yanasaidia kauli yake kwamba alikuwa mwana wa Mungu. Alikuwa na ushahidi wa Yohana, mbatizaji, lakini ushahidi aliouzungumzia katika Yohana 5:32 ilikuwa ni Mungu mwenyewe.

Yohana 5:36-37, "*Lakini ushuhuda nilio nao mimi ni mkubwa kuliko ule wa Yohana; kwa kuwa zile kazi alizonipa Baba, ili nizimalize, kazi hizo zenyewe ninazozitenda, nazishuhudia ya kwamba Baba amenituma. Naye Baba aliyenipeleka amenishuhudia, sauti yake hamkuisikia wakati wo wote, wa sura yake hamkuiona.*"

Yesu alipobatizwa na Yohana, Mungu, mwenyewe alifanya ifahamike kuwa Yesu alikuwa mwanaye mpendwa.

Math. 3:16-17, "*Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*"

Mungu alikuwa shahidi mwingine wa Yesu katika Yohana 5:32, sio wale wa wakati wa mwisho.

Kati ya kufufuka kwake na kupaa kwake kwa ajabu, Bwana alisema katika Luka 24:48 na Matend. 1:8, kama ifuatavyo:

- Luka 24:48, "*Ninyi ni mashahidi wa mambo haya.*"
- Matend. 1:8, "*Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi.*"

Kauli kama hii haiwezi kuendana nay a mashahidi wa leo wa Kristo kwa namna yoyote ile na kwa kufikiria kwa mtu.

Unapaswa uelewe kwamba Yesu alisema kuwa wao, mitume, walioishi kipindi kile wata "*pokea nguvu, baada ya Roho Mtakatifu kuwaijilia juu yao.*"

Wakati Yesu alimtokea Sauli katika njia ya kwenda Dameski, alimwambia, katika Matend. 26:16, "*Lakini inuka usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayo nitajidhihirisha kwako;*"

Paulo alitakiwa kumuona Yesu kabla ya kuwa na sifa ya shahidi.

Ni jinsi gani kuna utofauti mkubwa kutoka katika siku za kisasa za leo katika karne yetu!

Ni wangapi leo wamemuona Yesu ana kwa ana? Hakuna, rafiki yangu; hakuna hata mmoja!

Utambulisho Wa Mitume Wa Ushahidi

Hebu tuangalie jinsi mitume walivyotumia neno **mashahidi,** baada ya Yesu kurudi mbinguni.

Katika kumchagua mmoja ili achukuwe nafasi ya msaliti aliyeanguka, walitangaza, katika Matend. 1:21-22, *"Basi katika watu waliofuatana nasi wakati wote Bwana Yesu alipokuwa akiingia na kutoka kwetu, kuanza tangu ubatizo wa Yohana, hata siku ile alipochukuliwa kwetu kwenda juu, inampasa mmoja wao awe shahidi wa kufufuka kwake pamoja nasi."*

Ni jinsi gani inavyopendeza, hii inasikika kama "mashahidi" wa leo kwa Mungu na kwa Yesu? Jibu liko wazi!

Petro na Yohana hakika walikuwa mashahidi wa Bwana.

Walisema katika Matend. 4:19-20, "*Petro na Yohana wakawajibu wakawaambia, kwamba ni haki mbele za Mungu kuwa sikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; maana sisi hatuwezi kuacha kunena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*"

Tamko hili haliwezi kusemwa na wanaodai kuwa ni mashahidi wa Mungu na Yesu Kristo. Wanachokifanya wanalilia mbali kwaku sema kile Petro na Yohana walicho andika, kama ushahidi uliyoandikwa kuhusu Yesu. Wanaongelea jinsi wanavyo jisikia na ujuzi wao.

Mbele ya kuhani mkuu, mitume walisema katika Matendo. 5:32, "*Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio.*"

Biblia inasema sisi tu *"Mashahidi"*; lakini wakina nani waliokuwa *"sisi"* ambaye alikuwa akizungumzia.

Mazingira yana mdhihirisha wasemaji kuwa ni mitume. Hakuna shaka juu ya hili!

Katoka nyumba ya Kornelio, Petro aliweka wazi, katika Matend. 10:41, "*Si kwa watu wote bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu ndio sisi tulio kula na kunywa pamoja naye, baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu.*"

Je "*mashahidi"* wowote hasa leo waliochaguliwa na Mungu, wako kama hawa waliokuwa wakati wa Biblia? Inaweza kusemwa juu yao kwamba kweli wali *"kula na kunywa pamoja naye alipofufuka kutoka katika wafu"?* Jibu liko wazi na kinyume, "Hapana!"

Katika Matend. 4:33, Luka anasema, "*Na kwa nguvu nyingi aliwapa mitume ushahidi wa kufufuka kwa Bwana Yesu: Na neema nyingi ikawa juu yao wote.*"

Ni nani aliyetoa ushahidi? Mitume!

Lakini, hufahamu, kwamba hatuna mitume leo- hakuna! Hakuna mtu yeyote leo aliyemwona Bwana, au kushuhudia kufufuka kwake!

Hakuna Mashahidi Wa Mungu Leo

Katika ulinganifu wa ghafla, naleta baadhi ya njia ambazo mashahidi wa leo wanatumia katika kazi zao za ushahidi.

Baadhi wanadai kuwa ni mashahidi wa Mungu; lakini, Biblia inasema katika Yoh. 1:18, "*Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote, Mungu mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.*"

Madai kama hayo, leo hii ni ya uongo!

Hata kama kungekuwa na mashahidi wa kweli wa Mungu katika ulimwengu wetu leo, hakika wasinge kataa ukuu wa Yesu na kwa hivyo wanamfanya awe mwanadamu aliyeumbwa.

Biblia inasema, katika Yoh. 14:8-11, "*Filipo akamwambia Bwana utuonyeshe Baba yatutosha, Yesu akamwambia mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yang? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake. Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu; la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe.*"

Marafiki zangu, hakuna mwingine isipokuwa Uungu unaweza kusema udhibitisho wa kweli- shahidi wa kweli wa Mungu! Hakuna shahidi kama huyo wa Mungu, au Kristo, katika dunia leo!

Watu wengi leo wanafikiria wao wenyewe kuwa mashahidi wa kisasa wa Bwana. Lakini, tena nauliza, ni wangapi leo wanaoishi waliomuona Yesu kabla ya kufa kwake? Kuna ye yote aliyemwona wakati wa kufufuka kwake na kutokea kwake iliyo onyeshwa katika shemu za mwisho za Mathayo, Marko, Luka, au Yohana? Hakuna, rafiki yangu! Hata mmoja!

Je mtu ye yote amewahi kumuona Yesu katika mkutano maalum, kama Sauli wa Tariso, ilivyotajwa katika Matend. 9? Bila shaka hakuna!

Je yeyote amewahi kumuona Yesu, kama Yohana, mtume alivyo muona katika kisiwa cha Patimo, karibia mwisho wa karne ya kwanza? Hapana!

Mashahidi wa leo wamevuviwa? Hapana!

Je kuna mtu yeyote aliyepokea agizo binafsi kutoka kwa Kristo ili aweze kuwa na sifa ya kuwa shahidi wa Bwana? Hakika hakuna!

Kwa kusekana kwa sifa sahihi na kukoswa ujuzi wa Biblia, hakuna chochote kifupi cha kushangaza kuangalia jinsi gani watu wengi wanaweza kuwa hao wanaodai kuwa ni mashahidi wa leo wa Yesu!

Mkanganyiko Wa Mashahidi

Rafiki yangu, nakuuliza kama leo mashahidi wa kisasa wameitwa na Bwana kwa ushahidi wake, kwa nini wanajichanganya wao kwa wao sana, na wote pia wana changanya Biblia?

Ni dhahiri kwamba “mashahidi” wa kisasa wa Mungu na Yesu Kristo wanatoa ushuhuda unao fanana. Ushahidi wao mara nyingi uchanganya sana.

Wale wanaojitangaza kuwa ni mashahidi wa kisasa wa Yesu Kristo, karibia bila udhuru, wanaamini kuwa wana neema binafsi waliopewa kufanyia kazi (kulingana na vipimo vyao wenyewe) utendaji kazi wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa na munganiko wa moja kwa moja katika mioyo yao.

Wengi wao wanahisi kwamba Roho anawaongoza moja kwa moja na ushahidi wao ni halali kama maandiko ya Mungu na udhihirisho wa ushuhuda wao ulivyofunuliwa katika Biblia.

Hakika, mashahidi wa kisasa maranyingi wanaweka ushahidi wao juu na zaidi ya Biblia kwa sababu wanapenda kulinganisha hisia zao na ujuzi juu ya kile Biblia inasema.

Mmoja wa kaka yangu binafsi alifanyika mkatholiki kwa sababu ya ujuzi wake wa “mwamba wa joto”. Alisema aliona isivyokawaida mwamba ulio lala chini na akalichukuwa. Akasema kwamba ilikuwa ni ya moto kwamba alikuwa karibu kuitupa. Akadai kwamba alikuwa ni Mungu anampa ujumbe kwamba aliitajika afanye kitu kuhusiana na maisha yake ya kiroho, na kwa vile alipata jiwe karibia na Kanisa la katholiki, alifikiria Mungu alimwambia hapo ndipo alipoitaji kuwa. Haikuwa ni mandiko ya Mungu matakatifu yaliyomwambia anapopaswa kuwa.

Mashahidi Wa Kweli Wakiwa Na Ushuhuda Wa Kweli

Kitabu cha Matendo ya Mitume ni kitabu cha Wokovu.

Mitume walikitegemea katika kuhubiri injili kuwaokoa watu; siyo kwa kusema kuwa na mwamko wa hali ya juu ambayo huanzia mwanzo na mwisho.

Mitume walitegemea zaidi katika ukweli kuwa sogeza watu katika kuitii injili.

Siku ya Pentekoste, Matendo, sura ya 2, mitume wakitoa ushahidi uliovuviwa ya Kristo na injili Yake.

Katika Matendo 2:37, imesemwa, "*Walipo yasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu.*"

Lazima uangalie kwamba Biblia inasema, "walipo yasikia haya" – **siyo** walipo "hisi haya."

Ikiwa mashahidi wa leo wameagizwa kumshuhudia Bwana Yesu Kristo, tuna baathi ya maswali ambayo yanaweza kuwa na majibu magumu:

Kwa nini *"mashahidi"* wengi hawajui jibu la Biblia kwa swali, *"Ni fanye nini ili niokoke?"*

Kwa nini wengi wao hawajaitii injili, kama watu walivyo fanya wakati wa Agano Jipya, waliposikia ushahidi uliovuviwa, ilivyofunuliwa katika kitabu cha Matendo ya mitume, wakati wa karne ya kwanza?

Kwa nini wengi wao huamini kuwa wokovu ni kwa "imani pekee"; lakini siku ya Pentekoste wakati watu 3000 walikuwa wanajibu wito uliyo andikwa katika Matendo. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."?*

Kwa nini mashahidi wengi leo wanafikiria Yesu atakuja kwenye mioyo ya wenye dhambi wakati mwenye dhambi akisema, "Bwana, niokowe"? vile vile hakuna ushahidi wa uvuvio kama huo, ikiahidi "Ondoleo la dhambi," inayo patikana kwenye Biblia kutoka katika ushahidi wa ukweli wa Bwana!

Lakini, hebu na tuangalie swali lingine: Kwa nini *"mashahidi"* wa sikuhizi wachache wanaonekana hawajui kitu chochote kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu na kanisa la Bwana ambalo Yesu alilolifia?

Unajua, Agano Jipya inahusu habari hiyo yote!

Mandiko , ushahidi uliyovuviwa wa Mungu, kila mara, bila upendeleo, inaongea kwa ufasaha kuhusu mambo haya.

Lakini, *"mashahidi"* wa sasa wanajua kidogo kuhusu maandiko ukihusisha na mambo haya, na mara nyingi wana kana, au wana kataa kukubali kile walicho onyeshwa. Tofauti iliyoje!

Kwa nini "*mashahidi"* wa leo wamevutiwa sana katika kuisi kwao na ujuzi wao badala ya kujihusisha na jinsi watu walivyo kuwa wakiokolewa katika Biblia; watu kama wale wa siku ya Pentekoste, ambao nimewazungu mzia?

- Au, kama mfano wa Towashi, katika Matend. 8
- Au mlinzi wa gereza, katika Matend 16?
- Au Sauli, Matend 9?
- Na wengine wengi walioandikwa katika kitabu cha Matendo?

Umeshawahi kusikia kuhusu *"mashahidi"* waliotaka kutumia wokovu, uliyoandikwa katika Matendo, kama mfano wa wokovu na mifano ya ukweli wa mashahidi wa Bwana?

Kwa nini hakuna mvuto kati ya *"mashahidi"* ukizingatia kitabu, sura na misitari inayohubiri kutoka katika Biblia?

Haya ni maswali ambayo "*mashahidi"* wa siku za leo hawawezi kujibu.

Suluhisho la tatizo ni nini?

Tunaitaji kurudi katika Biblia na tuongee pale inapo ongea, na tunyamaze pale inaponyamaza; tuite vitu vya Biblia kwa majina ya kibiblia na kufanya vitu vya Kibiblia katika njia za Kibiblia.

Tunatakiwa kuzungumza kama maandiko yanavyo elekeza, kama Petro alivyoamuru katika, 1 Petro 4:1, "*Mtu akisema, akisema na aseme kama mausia ya Mungu ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.*"

Kuna hitaji kubwa leo kurudi katika mafundisho na mienendo ya Agano Jipya

Tunatakiwa turudi katika mahubiri na mafundisho yaliyo fanywa kati ya karne ya kwanza na mashahidi wa kweli wa Kristo.

Tunatakiwa turudi katika mienendo ya kanisa la Agano Jipya katika shauku yake ya kuhubiri injili kwa waliopotea na kuwa na mapenzi mema ya kuwa saidia wale wenye itaji.

Tunatakiwa kushikamana katika kuwatunza walio okolewa, wawe wameokoka.

Hitimisho

Ulimwengu leo unaitaji injili ya Kristo; uwakilishi ukweli uliyovuviwa, ukweli wa injli na si cho chote bali ukweli! Lakini kumbuka, ukweli uliovuviwa na ushuhuda unatokana na ukweli ushahidi ulioruhusiwa unaopatikana katika Biblia!